Burundi — nchi ya pili katika Bara la Afrika — kuunda taasisi ya Kiswahili — Kenya itafatia

NA KAMAL KHAN

...KA Mhadhara wa ...wahili wa Kimataifa ...lianyika mapema mwezi huu ...ika Kenya Polytechnic, ...obi, mmoja wa wajumbe ...ka nchi za kigeni Bwana ...omwami Marcel kutoka ...chi ya Burundi. Bwana ...ye ni mtaalamu wa Kiswahili ...msimamizi mkuu wa Taasisi ...Kiswahili ya nchi hiyo.

...tika hotuba yake alieleza ...ya Kiswahili ilivyokuwa ...na ilivyo leo. Alisema ...Warudi toka enzi Ujeru... na Ubeljigi walikuwa ...mia Kiswahili kama lugha ...pili kwa sababu ya ...siliano na nchi jirani. Leo ...ile Burundi ni nchi huru, ...dhali kubakia nyuma katika ...mbo wa maendeleo ya ...engu.

...ra ya lugha ya Kifaransa ...kuwa ikifunzwa na ...eljigi, Warundi leo ...endeleo kujifunza pamoja ...Kiingereza na Kiswahili pia. ...hivyo, Kiswahili ni lugha ...kigeni inayotumika na ...tumika sana sokoni, ...dukani, barabarani, ...ndani na ofisini. Viongozi ...hukitumia kuandika na ...ea hotuba zao. ...angazo ya habari kwa ...wahili yanachukua sehemu ...kubwa ya redio ya Burundi.

...ngu zanani Kiswahili ...kuwa kikifunza katika shule ...msingi kwa watoto wa ...lamu hata baadhi ya watu ...walikichukulia kuwa ni lugha ...Waislamu mpaka walipoto... ...wa na kufahamikiwa kuwa ...chombo cha maana cha watu ...kuwasiliana kwa urahisi.

...maarufu wa Kiswahili leo ...mesitanya kufundisha katika ...shule za msingi, upili, vyuo vya ...ndi, chuo kikuu cha Kiraia ...chuo kikuu cha Kijeshi.

Sehemu ambayo bado haijaanza kutumia Kiswahili ni mageziti.

Burundi ina magezeti mawili, la Kiburundi na la Kifaransa. Hakuna bado gazeti la Kiswahili kwa sababu mpaka hadi hii hakuna waandishi waeledi wa habari kwa Kiswahili kwa utangazaji magazetini. Magazeti ya Kiswahili yapatikanayo Burundi ni yale yaagizwayo kutoka nchi za Africa ya Mashariki na Zaire

Kitendo cha pekee kinachotendeka Burundi ni kuwa katika siku maalumu za taifa maombi ya dini ya Kikatoliki, Kiprotestani na Kiislamu huendeshwa hadharani kwa Kiswahili. Padri wa Kikristo akiwa anaendesha maombi, Waislamu waweza kushiriki ikiwa wayafahamu maombi au wananyamaza, na Sheikhe wa Kiislamu anapoleta dua, Wakristo nao pia waweza kuwandama au kumnyamaza mpaka amalize. Kwa hivyo, si Kiswahili tu, bali dini pia ni miongoni mwa vyombo vya kuwajumuisha Warudi kama taifa moja lenye mwelekeo mmoja.

Na shule za ngumbaro leo, ziko na zinawafunza watu wazima Kiswahili kwa sababu wao nao hawataki kuwachwa nyuma katika mkumbo wa maendeleo ya nchi na ya ulimwengu kwa jumla.

Burundi imekuwa nchi ya pili katika bara la Afrika kuanzisha Taasisi ya Kiswahili kukiimarisha Kiswahili, Tanzania ikiwa ya kwanza na Kenya kutarajiwa kuwa ya tatu mwaka wa 1983. Taasisi hii ya Burundi karibu itakuwa na makao yake maalumu katika Jumba la Utamaduni linalojengwa katika mji mkuu wa Bujumbura.

Jumba hili lina sehemu tatu: ya Utamaduni, ya Kiburundi, ya Dini ya Kiislamu na ya Kiswahili. Gharama ya kulijenga Jumba hili imetolewa na Rais Muammar Ghaddafi wa Jamhariya ya Libya.

HATUJAPATA KIONGOZI BADO

SISI wakazi wa huku Pwani, mpaka dakika hii bado hatujakuwa na mjumbe, awe diwani ama mbunge ambaye angestahili kuitwa Kiongozi. Hawa madiwani na wabunge tulionao sasa hivi, hawastahiki kuwaita hata wawakilishi wa watu licha ya kuwaita viongozi.

Pengine baadhi ya watu hawaelewi tofauti baina ya mwakilishi na kiongozi. Mwakilishi ni mtu muliyemchagua ili ende akepeleka mbele maoni yenu, yaani ende akawasemee.

Na kiongozi ni mtu ambaye ana kipaji cha kuongoza, anaweza akaonyesha watu madhara na ubaya wa jambo linaloendelea kutendwa bila ya kuogopa matokeo.

Hapa Pwani tuna maovu mangapi na shida ngapi na hakuna mtu anayesema lolote. Wakati wa Uchaguzi ukifika, wapiga kura hughilibika na mapeni ya miraa ama tembo na kwa hivyo wakafanya haraka ya kuamua mtu wa kumpa kura

Mara mtu huyu akisha chaguliwa, kazi yake ni kuanza kumchukia kiongozi huyu na yule na kuanza kutumiana matope kwenye mikutano.

Jee hiyo ndiyo kazi ya wabunge na madiwani wetu?

Ali Muhajiri,
MOMBASA.

POLE NDU YETU KHELEFU - WAVUTA BANGI HAWANA KHERI

...IWANI WA Kongowea ndugu Khelefu Salim ...mehukumiwa kifungo cha myaka mitatu. Hili ni tukio la ...huzunisha sana toka kwa madiwani wenzake, waihsani ...ake rafiki, zake na ni matungu makubwa kwa watu wake ...a nyumbani. Lakini si msiba wala si huzuni kwa wale ...wavuta bangi wasiokuwa na fikira wala busara.

Wewe huoni aibu kushikwa na bangi na tena ukenda ...bio kutafuta mtu kama diwani mwenye kazi muhimu za ... humizia wananchi ili aende akakudhamini, yaani ...achiliwe huru ili ukaendelee na kazi yako ya laana! Pekee ...kushikwa na bangi ni aibu kubwa kwa watu wenye busara ...zao. Avuliwaye nguo huchutama, na vipi watu hawa ...wasimama hadharani hata wakafika kuharibu heshima za ...madiwani.

Tukianza na hiyo bangi wenyewe, mwanzo wa mwaka ...huu tu kungia, Rais wa nchi hii Muheshimiwa Bwana ...Daniel Arap Moi alijitokeza na akalaani tendo la kuvuta ...bangi, kuiuza hiyo bangi na pia kuiotesha makondeni. Rais ...alifanya hayo kwa akili zake na kwa busara kamili. ...anafahamu kwamba iwapo watoto wataanza kufata ...mwenendo huo mbaya wa kuvuta bangi, akili zao ...zitaharibika na hawataweza kufanya maendeleo yoyote ...shuleni na hata katika maisha yao siku watakuwa ni watu ...kabisa kwani watakuwa ni wapungufu wa akili. Rais ...alijua kwamba iwapo hataanza kukataza vikali uvutaji wa ...bangi, basi raia wake wengi watapotea. Na kwa hivyo ...itakuwa ni hasara ya nchi mzima.

Rais akaanza kuwatimua Machifu nchini kote ili waanze ...kuyasaka makonde ya bangi na kuyaangamiza. Kwa kweli ...Machifu walifanya kazi kwa bidii kuyasaka makonde hayo, ...kuyachoma moto na kuwapeleka mahakamani wale ...waliyoyalima. Lakini tabia hii mbaya haimaliziki kwani ...kuna katika watu wale ambao wamefanya bangi kuwa ndio ...msingi wao wa maisha. Yaani kama vile watu wengine ...wanavyotegemea mahindi, miwa, ngano, chai, kahawa na ...mboleo, basi hawa nao ati huifanya bangi ndio kilimo cha ...kusafirisha nchi za nje na pia kutumia nyumbani.

Hatuwezi kumlamu diwani Khelef, kwani yeye hayo ...aliyoyafanya, hakuyafanya kwa kuwa yeye ni mvuta bangi ...wala kuwa anawaunga mkono hao wavuta bangi. Lakini ...alifanya wajibu wake wa kuokoa na balaa la kufungwa ...mtu wa huko sehemu yake. Ilikuwa ni lazima afanye hivyo. ...ikuwa ni lazima maana hapa Mombasa kazi za kuwapa ...madiwani na wabunge hatuzijuikamwe na badili yake ...mbunge ama diwani hufatwa ili akalipe bili ya taa au ...maji au karo ya shule au akwadhamini walaji miraa kwa ...mtu na kadhalika.

Khelef amefungishwa na wauza bangi wasiokuwa na ...busara. Kama wasingekwenda kutolewa, kura zingezuiwa ...hawa patemi diwani mwengine naye pia mumfungishe

MBUNGE WA BOMET BWANA SALAT AONGOZA AKINA MAMA

Bw. I. K. Salat akihutubu katika tafrija HIYO.
PICHA: FAHEEM PARKER.

KIKUNDI CHA kina mama wa kutoka bomet hivi karibuni kilifanya ziara ndefu na yenye shughuli nyingi Mombasa pamoja na sehemu kadha katika mkoa wa Pwani.

Mama hawa waliongozwa na Mbunge wao ambaye pia ni waziri mdogo katika ofisi ya Rais Mheshimiwa Bwana I. K. Salat.

Licha ya kutembelea sehemu mbali mbali mashuhuri mjini Mombasa ambzo ziliwavutia sana kina mama hawa pamoja na mbunge njoki wao walifanyiwa tafrija maalumu katika Hoteli mashuhuri mjini Mombasa, Lotus Hotel ambayo iliandaliwa na mwenye Hoteli hiyo Bw. Z. K. Nderu pamoja na mkewe Margaret nakudhuriwa na D.C. wa Mombasa Bw. Mugwe pamoja na wakuu wengine wa serikali Mombasa

PICHANI anaonekana Bw. Nderu akiwa na kikundi cha akina mama wa bomet.
PICHA: FAHEEM PARKER.

JISHINDIE

Miavuli maridadi katika shindano jipya la kujaza maneno



JINA ....

SANDUKU LA POSTA ....

....

SWAHILI CROSSWORD NO. 129

KWENDA KULIA:

1. Sehemu iliyo na nafasi katika nyumba
4. Ufupi wa bibi
5. Kivazi cha kike
7. Sehemu karibu ya shingo
8. Ama
9. Upwa
12. Ndege mwenye thamani
13. Kiungo cha maneno
14. Sehemu ya mbele ya chombo
15. Toa moshi kwa kinga
17. Sehemu moja ya kumi ya mia
18. Ala, jalada

KWENDA CHINI:

1. Chakula kilicho ungua chini ya sufuria au chungu
2. Mtego wa samaki
3. Kama theluji
4. Sima ya makopa
6. Bora, nzuri zaidi
9. Hutengenezewa mito na magodoro
10. Aina ya majani
11. Jina la Kijaluo
12. Chombo cha nyumbani
16. Neno la kumaka.

Washindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 128

1] Soody Nijamah, Sanduku la Posta 95712, Mombasa

2] Mrs. Nereya Oremo, Sanduku la Posta 33, Taveta

3] Mr. Petro M. Juma, Sanduku la Posta 30091, Nairobi.

Washindi waombwa wafike afisini mwa COASTWEEK

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 128 —

KWENDA KULIA:

1. MNYAPARA, 5. SA, 6. KIBABA, 7. LULU, 9. NAWA, 11. INI, 14. LALIMU, 15. NI, 16. LA, 17. PARAGA.

KWENDA CHINI:

1. MAKINDU, 2. ALAMA, 3. AWALI, 4. ASALI, 8. UNGUZA, 10. WALI, 12. VUNA, 13. TEMA, 15. NA.

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:

Uamuzi wa mauzi utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa.

Washindi watatu kila baada ya wiki mbili watapata miavuli maridadi. Shindano hili limedhaminiwa na COASTWEEK LIMITED, Mombasa.

Jawabu za Fumbo hili ziperekwe kwa Muhariri, COASTWEEK, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya Jumatano tarehe 4.11.81 saa nne asubuhi shindano hili litakuwa mwisho.